**MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI NDOGO LA MURANG'A MASHIRIKI**

**KIDATO CHA NNE**

**KISWAHILI, KARATASI 102/1- INSHA**

**JULAI, 2025**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

1. **Swali la lazima**

   Huu ni utungaji wa kiuamilifu. Vipengele viwili muhimu sana katika utungaji huu vidhihirike. Nayo ni:

   1. Umbo/ muundo/ sura
   2. Maudhui

1. **Umbo/ muundo/ sura**

   a) Umbo la kuandika barua memo libainike. Mambo yafuatayo yazingatiwe.

      I. Nembo -mfano kampuni ya Jitihada S.L.P 605-00200, MAJIMOTO
      II. Kwa- wafanyakazi wote
      III. Kutoka: Meneja
      IV. Mada: UKIUKAJI WA MAADILI YA KIKAZI
      V. Tarehe: 10/07/2025

   **b) Maudhui**

   Baadhi ya hoja ni kama zifuatazo:

      i. Kuchelewa kufika kazini kwa wakati unaofaa
      ii. Kutoka kazini mapema
      iii. Kukwepa majukumu waliopewa
      iv. Kutusiana
      v. Kuchumbiana
      vi. Kufanya mapenzi kiholela
      vii. Kuharibu mitambo ya mashine
      viii. Wizi wa vipuri
      ix. Wizi wa bidhaa za kampuni
      x. Kutowaheshimu wakubwa
      xi. Kuja kazini wakiwa walevi, n.k

      **TANBIHI**

      I. Atakayeandika sura tofauti au akose kuandika sura kabisa, atolewe ( alama 4 za sura)
      II. Akiandika maadili yanayokiukwa lazima aeleze adhabu zitakazopewa wakiukaji kwa kila mojawapo ya ukiukaji.
      III. Atakayekosa kuhusisha ukiukaji wa maadili ya kikazi na adhabu hatakuwa amejibu swali kikamilifu akadiriwe kulingana na mwongozo wa kudumu.
      IV. Watahiniwa wakadiriwe kulingana na vipengele mbalimbali vya mwongozo wa kudumu.

      **Swali la 2a**

      Umuhimu wa mitihani na tathmini

      i. Kupima uelewa wa mwanafunzi
      ii. Humsaidia Mwalimu kutathmini mbinu zake za kufunzia.
      iii. Kuhamasisha wanafunzi kusoma kwa bidi


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

iv. Kuwezesha kuwaweka wanafunzi katika viwango vyao vya uelewa
v. Kutambua vipaji na uwezo wa wanafunzi
vi. Ni nyenzo ya kuteulia
vii. Husaidia wazazi na walezi kuelewa maendeleo ya Watoto wao
viii. Mitihani ya kitaifa kama vile KCPE au KCSE hutoa tathmini ya jumla ya ubora wa elimu kwa taifa zima.
ix. Walimu hutathmini viwango vyao vya kufunza kutegemea malengo ya mtaala na silibasi.
x. Hutumika na taasisi za serikali kuwachagua watahiniwa katika kazi mbalimbali.

(kadiria majibu mengine ya watahiniwa

**TANBIHI**

I. Mtanihiwa ana uhuru wa kuchagua aina ya insha atakayoiandika. Akadiriwe kulingana na uamuzi wake.
II. Hii ni insha ya hoja
III. Akadiriwe kuligana na ustadi wake wa kuelezea hoja kikamilifu na kutegemea vipengele vinginevyo katika mwongozo wa kudumu.

**Swali la 2b**

**Hii ni insha ya methali**

Maana ya ndani ya methali hii ni kwamba mtu anaposifiwa kupita kiasi kwa kazi au uwezo wake, anaweza kulegea, kuzembea au kuharibu kazi hiyo.

**Baadhi ya mikondo ya insha**

i. Mwanafunzi mwerevu darasani anasifiwa sana na walimu hatimaye anabadilika na kuanza utukutu unaomfanya kudidimia masomoni.
ii. Kiranja darasani anashushiwa sifa kemkemu na walimu Pamoja na mgomo shuleni.
iii. Kiongozi wa taifa anapewa tuzo ya kimataifa hatimaye anawanyanyasa raia wanapomchagua tena, n.k.

**TANBIHI**

I. Mtahiniwa aandike kisa kinachodhihirisha ukweli wa methali hiyo.
II. Methali huwa na sehemu mbili. Sehemu ya wazo na sehemu ya jawabu sharti


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

sehemu zote mbili zidhihirike. Mambo haya ni muhimu:

- ✓ Atakayeegemea upande mmoja asipite c+ (10)
- ✓ Ibainike kuwa mtahiniwa anaweza kuegemea sehemu ya pili kwa maneno machache tu, kishazi au sentensi.

  iii) Atakayeandika visa akadiriwe kulingana na viwango mbalimbali katika mwongozo wa kudumu.

**Swali la 2c**

Hii ni insha ya mdokezo. Huu ni mdokezo tamati. Mtahiniwa atangulize kisa kitakachomalizikia kwa maneno ya mdokezo.

Taswira hiyo ya uharibifu, maangamizi na vifo iamabatanishwe na matukio asilia.

Matukio asilia yaliyosababababishwa pengo hilo baina ya vijana au rai ana utawala wa taifa la Zahama yaelezwe.

Mpwito wa wakati ambao kileleta chake ni hali hiyo uambatanishwe.

**TANBIHI**

1. Atakayekosa kumalizia kwa maneno ya mdokezo ni kosa ndogo tu la mtindo akadiriwe kulingana na mwongozo wa kudumu.
2. Atakayeanza kwa maneno ya mdokezo amepungukiwa kimtindo akadiriwe kulingana na viwango mbalimbali vya mwongozo wa kudumu.
3. Atakayeandika kisa kisichohusiana na maneno ya mdokezo hatimaye ayapachike amepotoka kimaudhui (3/20) atuzwe D
4. Mtahiniwa akadiriwe kwa kuzingatia viwango mbalimbali vya mwongozo wa kudumu.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes